# Maswali na Majibu Kuhusu UVIKO-19 Chanjo kwa watoto



**Kwa nini watoto miezi 6 na zaidi wapate chanjo dhidi ya UVIKO-19?**
Watoto wanaopata UVIKO-19 wanaweza kuugua sana na kuhitaji matibabu hospitalini. Chanjo zinaendelea kutoa kinga nzuri dhidi ya matokeo mabaya zaidi ya UVIKO-19. Kuchanja watoto pia kunaweza kuwapa wazazi imani zaidi kwa watoto wao kushiriki katika sehemu za kulelea watoto, shule, na shughuli nyingine.

**Je, watoto wanahitaji chanjo moja au mbili?**
Watoto na vijana wanahitaji chanjo mbili. Watoto miezi 6 na zaidi hupata dozi ndogo kuliko vijana na watu wazima.

**Kwa nini watoto wanapata dozi ndogo?**
Kinga zao za mwili ni tofauti na watu wazima. Dozi ya chini hutoa kinga nzuri sana dhidi ya UVIKO-19.

**Tunapaswa kusubiri kwa muda gani kati ya dozi ya kwanza na ya pili kwa watoto?**
Watoto wanapaswa kusubiri angalau wiki nane kati ya dozi yao ya kwanza na ya pili.

**Je, chanjo ya UVIKO-19 inaweza kuathiri kubalehe au uzazi kwa watoto?**
La. Hakuna ushahidi au sababu za kisayansi kuamini kuwa chanjo ya UVIKO-19 itaathiri kubalehe au uzazi.

**Mtoto wangu alikuwa na UVIKO-19. Je, mtoto anaweza kupata chanjo** ya **UVIKO-19**?
Ndiyo, mtoto wako anaweza kupata chanjo wiki nane (miezi 2) baada ya kupata UVIKO-19. Chanjo hiyo bado itasaidia kuwakinga na magonjwa kwa baadaye.

**Tunapaswa kusubiri kwa muda gani kati ya chanjo ya UVIKO na chanjo zao za umri wa kwenda shule zilizopangwa?**
Watoto watahitaji dozi mbili za chanjo ya UVIKO angalau wiki nane kati yazo na watachukuliwa kuwa wamechanjwa kikamilifu siku 14 baada ya dozi yao ya pili. Mtoto anapaswa kusubiri siku 14 kabla au baada ya chanjo ya uviko-19 kupataa chanjo za kawaida isipokuwa kama itashauriwa vinginevyo na mhudumu wa afya.

**Je, mtoto wangu au mimi tunaweza kupata UVIKO -19 ikiwa tuliugua hapo awali?**
Ndiyo, wewe au mtoto wako mnaweza kupata UVIKO-19 ikiwa mliugua hapo awali, haswa na Omicron. Chanjo inakupa kinga zaidi, hata kama tayari ulikuwa na UVIKO. Chanjo inaweza kusaidia kuzuia magonjwa mabaya na kifo ikiwa utaambukizwa tena.

**Vikwazo vingi sasa vimeondolewa. Je, hiyo inamaanisha kuwa UVIKO-19 haupo, au sio hatari tena?**

Immigrant Services
Association of Nova Scotia
isans

Hapana, UVIKO-19 bado upo. Bado ni hatari kwa wazee na watu wenye magonjwa sugu, hasa ikiwa hawajachanjwa. Pia bado ni muhimu kufuata miongozo ya afya kama vile kuvaa barakoa kwenye mazingira ya ndani, kunawa mikono mara kwa mara, kufunika mdomo wako unapokohoa, na kupata chanjo.

**Uthibitisho wa chanjo hauhitajiki tena kushiriki katika matukio yasiyo muhimu. Kwa nini basi watoto wangu au watu wazima wapate chanjo?**
Chanjo inakukinga na ugonjwa mbaya na kupunguza hatari yako ya kuupitisha kwa wengine. Kupata chanjo husaidia kulinda watoto wako, marafiki zako, na jamii yako. Baadhi ya shughuli na ajira zitaendelea kuhitaji uthibitisho wa chanjo (kama vile wahudumu wa afya, walimu, wageni wa hospitali, n.k.). Kwa kuongezea, ikiwa unataka kusafiri, lazima uwe umechanjwa kikamilifu kwenda maeneo mengi nchini Canada na ulimwenguni.

**Je, chanjo inaingia kwenye vinasaba vya mwili wa binadamu? Nimesikia hadithi nyingi kwamba chanjo inaingilia mabadiliko ya jeni katika mwili wa binadamu.**
Hapana, chanjo ya mRNA haiathiri vinasaba vyako. Haiingii hata kwenye kiini cha seli.
Chanjo inapoingia mwilini mwako, inazifundisha seli jinsi ya kutengeneza protini ambayo itasababisha mwitikio wa kinga ya mwili wako. Haiwezi kuwa sehemu ya seli au kuishi katika seli zako.

**Kwa nini baadhi ya watu hupona lakini bado wanaonekana kuwa na ugonjwa wanapopima?**
Mtu ambaye amethibitika kuwa na UVIKO-19 anaweza kupima na kipimo cha PCR na akaonyesha kuwa ana ugonjwa kwa hadi siku 90 baada ya kuambukizwa. Hii ni kwa sababu PCR inaweza kugundua kiasi kidogo cha virusi. Hii haimaanishi kuwa bado unaambukiza.

**Ikiwa mtoto wangu ana kinga dhaifu ya mwili, je, anastahili kupata dozi ya ziada?**
Ndiyo, watoto walio na kinga dhaifu wenye umri wa miezi 6 hadi miaka 4 wanaweza kupata dozi moja ya ziada ya chanjo ya UVIKO-19 ya Moderna siku 56 baada ya dozi ya pili. Watu walio na kinga dhaifu (miaka 5 au zaidi) wanaweza kupokea dozi moja ya ziada ya chanjo ya UVIKO-19 ya mRNA siku 56 baada ya dozi ya pili.

**Watoto wangu wanaweza kupata wapi chanjo ya UVIKO-19?**
Katika duka la dawa, kliniki ya chanjo ya bila miadi, au IWK.

**Mtoto wangu anawezaje kupata chanjo?**
Kabla ya kuanza:
1. Unahitaji kadi halali ya afya ya Nova Scotia ya mtoto wako ili kuweka miadi mtandaoni.
2. Unahitaji namba ya simu endapo italazimu kuwasiliana nawe.
3. Toa barua pepe wakati unaweka miadi. Utapokea barua pepe ya uthibitisho wa miadi, barua pepe ya kukumbusha siku moja kabla ya miadi, na barua pepe baada ya miadi na rekodi ya chanjo ya mtoto wako.

Jinsi ya kuomba miadi:
Unaweza kuweka miadi ya chanjo ya Uviko-19:
- Mtandaoni kwa kliniki: https://novascotia.flow.canimmunize.ca/en/covid-flu-booking
- Kwa simu kwa kupiga namba 1-833-797-7772 (Jumatatu hadi Ijumaa, saa 1 asubuhi hadi saa 1 jioni na Jumamosi hadi Jumapili, saa 4 ashubuhi hadi saa 12 jioni). Unahitaji kupiga simu kutoka kwenye nambari ya simu ya Canada na uwe Canada unapopiga simu. Ikiwa mteja anahitaji ukalimani, hii ndiyo njia bora ya kuweka miadi (angalia "Huduma za Ukalimaini zinazopatikana" hapa chini)

Kwa taarifa zaidi, angalia ISANS Jinsi ya kuomba miadi ya chanjo kwenye tovuti ya Mradi wa Beacon.

Immigrant Services
Association of Nova Scotia
isans

Jinsi ya kupata Kliniki ya Bila Miadi

Chanjo pia hutolewa kwenye kliniki mbalimbali za kwenda bila miadi. Sehemu hizi na nyakati hizi hubadilika wiki hadi wiki.  Unaweza kupata orodha mpya zaidi ya kliniki za kwenye jumuiya hapa: https://www.nshealth.ca/drop-in-vaccine-clinics.

Maduka ya dawa pia hutoa kliniki za bila miadi: https://pans.ns.ca/walk-covid-19-vaccine-clinics

Huduma za Ukalimani zilizopo

Ikiwa mteja anahitaji huduma kwa lugha nyingine isipokuwa Kiingereza, anaweza kuomba mkalimani anapoweka miadi yake kwa simu **1-833-797-7772** (zaidi ya lugha 125 tofauti zinapatikana). Mtaalamu atapitia maswali yote ya afya na uchunguzi pamoja na wateja kujibu chochote kinachowapa wasiwasi na kusita waliko nako kuhusu chanjo.

Maduka ya dawa pia hutoa vipeperushi kwa lugha tofauti ambavyo wateja wanaweza kusoma wanapopata chanjo zao. Kunaweza pia kuwa na wafanyakazi sehemu hizo ambao wanaweza kukalimani.

**Coronavirus (UVIKO-19)**
**Chanjo ya UVIKO-19**
**Usalama wa chanjo na madhara yanayowezekana**
**Chanjo ya UVIKO-19: Mwongozo wa Kinga wa Canada**
**Chanjo ya UVIKO-19 kwa watoto na vijana**
**Maswali yanayoulizwa mara kwa mara kuhusu Chanjo ya UVIKO-19 | CDC**

Immigrant Services Association of Nova Scotia
isans